KIJARIDA KUHUSU

# UTETEZI KATIKA JINAI

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp
ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

KIJARIDA KUHUSU

# UTETEZI KATIKA JINAI

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO


1. UTANGULIZI ........................................................ 10
2. MAANA YA JINAI ........................................................ 10
3. ADHABU YA MAKOSA YA JINAI ........................................................ 11
4. UENDESHWAJI WA KESI YA JINAI ........................................................ 12
5. UTETEZI WA KESI YA JINAI ........................................................ 12
   5.1.Upunguani au Kichaa ........................................................ 13
   5.2.Ulevi wa Kupindukia ........................................................ 13
   5.3.Kukosea Ukweli ........................................................ 14
   5.4.Kulinda Mali, Nafsi Yako Mwenyewe au Nafsi ya Mwingine ........................................................ 15
   5.5.Kuchukizwa Kupita Kiasi ........................................................ 16
   5.6.Umri ........................................................ 18
   5.7.Kushurutishwa ........................................................ 19
   5.8.Nia njema ........................................................ 19
   5.9.Kinga ya kisheria ........................................................ 19
6. HITIMISHO ........................................................ 20

## SHUKRANI

Tunatoa shukrani kwa wanasharia wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la tatu hususan Wakili Harold Sungusia, Wakili Fulgence Massawe, Wakili Jeremiah Mtobesya, Bw. Rodrick Maro na Bw. Evans Sichalwe, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania mnamo Septemba, 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu

ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa utakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa sheria.

## DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma yakusaidia jamii ya watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pam oja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndio maana basi Kituo kimeamua kutoa machapisho haya na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelekezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika vijitabu hivi tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapopata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi

ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia. Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafahdhali umsaidie na mwenzako kupata usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

## 1. UTANGULIZI

Ndugu wasomaji maada hii itazungumzia kimsingi aina za utetezi katika makosa ya jinai. Ni muhimu kuzieleza aina mbalimbali za utetezi katika makosa ya jinai kwa kuwa tofauti na mashauri ya madai, makosa ya jinai huandamana na adhabu kali. Basi ni vyema jamii ikajulishwa kwa ndani zaidi jinsi ya kujitetea katika makosa ya jinai.

## 2. MAANA YA JINAI

Jinai ni makosa ambayo yamekatazwa na sheria kwa kuwa yana madhara kwa jamii. Katika makosa ya aina hii muathirika ni dola na mkosaji huadhibiwa kwa faini, kifungo au adhabu yeyote nyingine iliyoainishwa na sheria. Hivyo makosa ya jinai yameorodheshwa katika Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 na sheria mbalimbali za nchi. Makosa hayo ni kama vile wizi, ubakaji, shambulio la kudhuru mwili, jaribio la kutaka kujiua n.k.

Kama ilivyoelezwa, muathirika wa makosa ya jinai ni dola kwa vile dola ndio inayobeba dhamana ya usalama wa raia. Kwa hiyo mamalaka ya kushtaki mtu aliyetenda kosa la jinai ni Jamhuri. Hata hivyo mara nyingine muathirika halisi wa kosa la jinai ni raia au mtu binafsi aliyetendewa kosa la wizi, mauaji au ubakaji. Muathirika halisi wa kosa la jinai huitwa muathirika wa jinai au mlalamikaji au mhanga.

## 3. ADHABU YA MAKOSA YA JINAI

Mtu yeyote anayetiwa hatiani kwa makosa ya jinai anaweza kupewa adhabu ya faini, kifungo au vyote viwili au kunyongwa mpaka kufa.

Pia adhabu nyinginezo zinaweza kutolewa; kama vile adhabu ya kutoa huduma kwa jamii, mtu kutoa fidia kwa mwathirika, kuchapwa viboko, kuonywa au kukaripwa au kutumikia kifungo cha nje.

## 4. UENDESHWAJI WA KESI YA JINAI

Katika makosa ya jinai, Jamhuri inamshtaki mtuhumiwa na kutoa ushahidi ili kuthibitisha tuhuma dhidi ya mshtakiwa. Mshtakiwa naye anapaswa kupeleka mashahidi wake mahakamani na kutoa utetezi wake dhidi ya shitaka analotuhumiwa. Pale ambapo mahakama itaona kwamba ushahidi dhidi ya mtuhumiwa ni mzito, basi mahakama itatoa kauli kwamba mtuhumiwa ana kesi ya kujibu/kujitetea. Hapa ndipo mtuhumiwa atatakiwa kujitetea kwa kutoa ushahidi alionao.

## 5. UTETEZI WA KESI YA JINAI

Mtuhumiwa anaweza kuwa ametenda kosa la jinai, lakini kutenda kwake kosa hilo kunaweza kuwa kumesababishwa na sababu ambazo sheria inatambua kuwa ni utetezi katika kosa hilo.

Utetezi huo ukikubaliwa mshitakiwa anaweza kufutiwa adhabu akapunguziwa adhabu au kutopatikana na hatia kabisa. Mazingira au sababu ambazo zinaweza kukubalika kisheria kuwa ni utetezi ni;-

**5.1. Upunguani au Kichaa**

Utetezi huu hutolewa pale ambapo mtuhumiwa atakuwa ametenda kosa lakini hakuwa anafahamu alichokuwa anakifanya kwa sababu ya kichaa au upunguani. Hii ina maana kwamba alitenda kosa hilo bila kukusudia.

**5.2. Ulevi wa Kupindukia**

Ulevi sio utetezi katika makosa ya jinai lakini mtuhumiwa akithibitisha kwamba wakati anatenda hilo kosa alikuwa amelewa kiasi cha kutofahamu nini alikuwa anatenda, anaweza ikawa sababu ya utetezi. Mtuhumiwa anatakiwa kuthibitisha kuwa hakuwa anakusudia kunywa pombe ili atende kosa la jinai.

### 5.3. Kukosea Ukweli

Kuna mazingira fulani fulani ambapo mtu anaweza kutenda kosa la kijinai kwa kukosea ukweli. Mfano; wakati wa usiku katika maeneo ambayo yana kawaida ya kuwa na nguruwe pori ambao hushambulia mazao ya wakulima; endapo mlinzi akiona mitikisiko ya mpunga akapiga tochi kwenye eneo hilo, na kuita kwa kusema kuna mtu hapa?, na endapo kama hakupewa jibu na endapo mwanga ni finyu sana kiasi hata kurunzi yake haikuweza kumuonyesha kama kulikua na mwanadamu amejficha eneo lile, basi endapo mlinzi huyu akirusha mkuki katika eneo husika akikusudia kumlenga nguruwe badala ya mwanadamu, basi hata kama mkuki ule ukimpata yule mwanadamu na kusababisha madhara kwake ikiwemo kifo, basi mshtakiwa katika mazingira

haya anaweza kutumia utetezi wa kukosea ukweli na ikithibitika ni kweli mahakama inaweza kumuachia huru bila adhabu yoyote.

### 5.4. Kulinda Mali, Nafsi Yako Mwenyewe au Nafsi ya Mwingine

Sheria ya makosa ya jinai inakubali utetezi kuwa mtuhumiwa aliua au alijeruhi kwa kujilinda mwenyewe/ kutetea nafasi yake au kulinda na kutetea mali yake au kumlinda na kumtetea mtu mwingine dhidi ya uovu wowote ule ambao sheria imeukataza. Utetezi huu ukikubaliwa na mahakama, basi mahakama itakuwa na jukuma la kumuachia huru mtuhumiwa. Hata hivyo utetezi huu una mipaka yake yaani matumizi ya nguvu dhidi ya uvamizi unaofanyiwa mtu au mali yake yasizidi kipimo

Kwa mfano mtu akikushambulia kwa fimbo si sahihi kujibu shambulizi au

kujikinga dhidi ya shambulio hilo kwa kutumia bunduki. Iwapo mshambuliwa atatumia bunduki au silaha nyingine ya moto, basi mahakama itaona kuwa matumizi ya bunduki hiyo kujibu shambulizi ni kutumia nguvu kupita kiasi.

### 5.5. Kuchukizwa Kupita Kiasi

Kuchukizwa kupita kiasi ni utetezi dhidi ya kitendo cha jinai kama vile kuua au kujeruhi. Ili mtuhumiwa aweze kukubaliwa ushahidi wake kuwa alikuwa amechukizwa kupita kiasi lazima athibitishe mambo yafuatayo;-

i. Kwamba alitendewa tendo ovu na la kudhalilisha, ambalo linamdhalilisha yeye binafsi au mtu yeyote ambaye ana uhusiano naye wa karibu mfano; mzazi wake, mke/mme, dada/kaka, mtoto, mwajiri au mtumishi;

ii. Maudhi yawe ya hali ya juu, yaani kama ni maneno yawe makali sana na ya kuudhi au kumdhalilisha mtu katika mambo fulani na kitendo kiwe cha papo kwa hapo yani ghafla ambapo mtu anakosa muda kwa kutuliza hasira;
iii. Awe amepatwa na hasira kupita kiasi kwa jinsi kwamba alipoteza uwezo wa kujitawala.

**Mfano**

Mtuhumiwa anapojitetea kuwa alifumania mkewe au mume akifanya ngona na mtu mwingine na hivyo akachukua hatua ya kumpiga na kumjeruhi vibaya huyo mtu mwingine au mwanandoa mwenzake, mahakama inaweza kuukubali utetezi huo kwa kuangalia uhusiano wa karibu uliopo kati ya wanandoa.

**Angalizo**

Ushahidi utakubalika tu iwapo mtuhumiwa atakuwa ametenda tendo la kupiga na kujeruhi muda huo huo bila kukawia alipowafumania wahusika yaani hapo kwa hapo. Katika mazingira hayo tajwa hapo juu mtuhumiwa anaweza akaachiwa huru na mahakama au kupunguziwa adhabu kwa utetezi huo.

## 5.6. Umri

Mtuhumiwa aliye chini ya umri wa miaka kumi hawezi kushtakiwa kwa kosal la jinai. Na iwapo ana miaka 12 mahakama haitamhukumu kuwa ametenda kosa hadi itakapohakikisha kuwa alitenda kosa hilo kwa kukusudia au alikuwa na nia ovu. Mtoto wa kiume wa miaka chini ya 12 anahesabika kutokuwa na uwezo wa kutenda kosa la kujamiiana.

### 5.7. Kushurutishwa

Mtuhumiwa anaweza kujitetea kuwa alishurutishwa na wenzake kutenda kosa la jinai kwa kutishiwa kuuawa au kuumizwa. Mahakama haitaukubali utetezi iwapo tishio la kuuwa au kuumizwa ni la wakati ujao.

### 5.8. Nia njema

Mtuhumiwa anaweza kujitetea kuwa alitenda kosa la jinai lakini alikuwa na nia njema.

### 5.9. Kinga ya kisheria

Mtu ambaye amekingwa na sheria kwa makosa ya kijinai kutokana na wadhifa wake hatashitakiwa kwa makosa ya jinai au akishitakiwa anaweza kujitetea kuwa anayo kinga ya kisheria kwa mfano, hakimu au jaji yeyote hatashitakiwa kwa kosa lolote ambalo atalifanya akiwa katika utekelezaji wa kazi yake.

## 6. HITIMISHO

Adhabu za makosa ya jinai zimeelezwa katika Sura ya 16 Sheria ya Kanuni za Adhabu. Sura hii imetoa ufafanuzi wa kila kosa na adhabu yake, pia imeeleza makosa mbalimbali ya jinai pamoja na adhabu zake.

Hata hivyo mahakama ndiyo yenye uwezo wa kutoa adhabu baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili. Baada ya kusikiliza utetezi huo mahakama inao uwezo wa kutoa adhabu kamili au kumpunguzia adhabu mtuhumiwa kulingana na utetezi wake ushahidi uliopo.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**
**(MAKAO MAKUU)**
Jengo la Jaji Lugakingira,
S. L. P. 75254, Kijitonyama, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz
**Tovuti:** www.humanrights.or.tz

**KITUO CHA MSAADA WA SHERIA**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

**OFISI YA ARUSHA**
Barabara ya Olerian, Olosiva,
Kitalu Na. 116/5, Sakina kwa Idd,
S. L. P. 15243, Arusha – Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**OFISI YA DODOMA**
Kitalu na 22. Area D,
S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*